HOTUBA YA MHESHIMIWA SOPHIA SIMBA (MB) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) KWENYE UZINDUZI WA MPANGO WA KIJAMII WA UHAWILISHAJI FEDHA KWA KAYA MASKINI, KIWANJA CHA MAILI MOJA KIBAHA, MKOA WA PWANI, 29 SEPTEMBA 2009

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhe. Hajat Amina Said Mrisho

Waheshimiwa Mabalozi na wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa

Waheshimiwa Wabunge

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Dkt. Servacius Likwelile

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Bi. Halima Kihemba

Menejimenti ya TASAF

Waheshimiwa Madiwani

Wawakilishi wa vyombo vya habari

Wageni waalikwa

Mabibi na mabwana

Awali ya yote namshuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha pamoja hapa katika uzinduzi wa Mpango wa Kijamii wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini.

Napenda kuchukua fursa hii kuushukuru uongozi wa TASAF chini ya Mkurugenzi Mtendaji, Dkt. Servacius Likwelile, kwa kunialika kushiriki katika shughuli hii.

Aidha nawashukuru wenyeji wetu kwa mapokezi mazuri na kwa kujumuika pamoja nasi. Asanteni sana.

Kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kuwakaribisha wageni wetu hususan, waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya kimataifa. Ninafurahi kwamba mmeweza kujumuika nasi, jambo ambalo linaashiria ukaribu na udugu uliopo baina ya nchi zetu, Taasisi zetu na wananchi kwa ujumla. Karibuni sana.

Ndugu wananchi
Kama mnavyofahamu nchi yetu inatekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), kwa kushirikisha wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya taifa hadi ngazi ya jamii.

MKUKUTA una lengo la kupunguza umaskini na kuweka kipaumbele katika kukuza uchumi, kupunguza umaskini wa kipato, kuinua hali ya maisha na ustawi wa jamii, na kuimarisha utawala bora. Mkakati huu unahimiza nchi kuwa na umiliki, uongozi wa serikali katika maamuzi, usawa na uratibu mzuri katika mchakato wa shughuli za maendeleo. Katika kuzingatia mikakati hii ya kupunguza umaskini, Serikali ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mwaka 2000.

Ndugu wananchi
TASAF ilianzishwa kupitia mkopo nafuu na utaalamu kutoka Benki ya Dunia. Moja ya madhumuni makuu ya TASAF ni kuhimiza na kuimarisha ari ya wananchi kushiriki na kuchangia, kwa kujenga uwezo wa kubaini, kuweka vipaumbele, kutekeleza, kusimamia na kutathmini shughuli za maendeleo yao. Njia hii itawezesha kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za jamii.

Ndugu wananchi
Walengwa wa TASAF kwa upande wa miradi ni jamii zenye uhaba wa huduma za msingi kama vile huduma za afya, shule na masoko. Vilevile kaya zenye uhaba wa chakula na makundi maalumu. TASAF huwezesha, huhamasisha na hujenga uwezo kwa makundi haya ya jamii maskini kuunda vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza.

Sote tunafahamu kuwa katika Tanzania tunazo kaya nyingi ambazo zipo kwenye mazingira hatarishi. Aidha UKIMWI umechangia kwa kiasi kikubwa, na hivyo kusababisha kaya nyingi zaidi kuwa miongoni mwa zile ambazo zimo katika mazingira hatarishi.

Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 6 ya watu wazima katika Tanzania wameambukizwa virusi vya UKIMWI.

Aidha karibu asilimia 12 ya watoto nchini ni yatima na idadi hiyo imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Watoto yatima na watoto walio katika mazingira hatarishi wameongeza jukumu kubwa zaidi kwa wazee, kwani kwa kiwango kikubwa wao ndio huhusika kulea na kuhudumia watoto hao.

Changamoto inayoikabili Serikali ni kuyafikia makundi na kaya zilizo katika mazingira hatarishi ili ziweze kunufaika kwa kupata huduma za jamii ambazo ni za msingi.

Ndugu wananchi
Naomba sasa nichukue fursa hii kuelezea juu ya uanzishwaji wa Mpango wa Kijamii wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini.

Kama tunavyofahamu, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alielezea kwenye hotuba yake ya uzinduzi rasmi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nne ni kuwashirikisha wananchi wote, kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kutokomeza umaskini. Alisisitiza umuhimu wa kujali maslahi na, mahitaji ya makundi katika jamii, wakiwemo watoto na wazee.

Kutokana na azma ya Mhe. Rais, Mpango wa Kijamii wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini ni moja ya mikakakti ya Serikali ya kuziwezesha jamii maskini kujiimarisha kiuchumi na kijamii.

Mpango huu umeanzishwa na Serikali ya Awamu ya Nne na unasimamiwa na TASAF kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, kwa ufadhili wa Serikali ya Japan kupitia Shirika la Japan Social Development Fund (JSDF) kwa lengo la kutimiza dhamira hiyo.

Nimefahamishwa kuwa, maandalizi yalianza mwaka 2006 ambapo maoni ya wadau mbalimbali kuhusu Mpango huu yalikusanywa toka mikoa ya Morogoro, Dodoma, Dar es Salaam na Pwani. Wadau waliohusishwa katika kutoa maoni juu ya uandaji wa Mpango huu ni pamoja na wanakaya kutoka katika kaya zilizo katika mazingira hatarishi, viongozi wa Halmashauri za Vijiji, wajumbe wa Kamati za Usimamizi za jamii, asasi zisizo za Serikali, Wizara mbalimbali na Idara mbalimbali za Serikali.

Vilevile Halmashauri za Wilaya za Morogoro, Bagamoyo, Kibaha na Dodoma na Mashirika ya Wadau wa maendeleo, hususani DFID, USAID, UNICEF, UNDP na ILO na washauri elekezi.

Maandalizi haya yalihusisha zaidi kupata maoni ya wadau, uandaaji miongozo, nyaraka, vitini vya mafunzo na mfumo wa taarifa wa komputa. Baada ya maandalizi ya awali kukamilika, utekelezaji wa mwanzo ulianza kuanzia mwezi Septemba 2008, ampapo uhamasishaji katika ngazi mbalimbali ulifanyika na mafunzo yalitolewa kwa wahusika.

Aidha, shughuli ya kuwapata walengwa ilifanyika na baadaye kupima uwezo wa utoaji huduma katika shule na zahanati. Na leo hii nafurahi kuwafahamisha kuwa Mpango uko tayari kuzinduliwa. Hongereni sana.

Naamini kuwa kaya zilizo katika mazingira hatarishi zitapatiwa fedha ambazo Serikali ya Awamu ya Nne imezitenga kwa ajili hiyo.

Ndugu wananchi

Ningependa kutumia fursa hii kuipongeza Menejimenti ya TASAF kwa kushirikiana na Halmashauri za Serikali za Mitaa kwa kuweza kupata mafanikio haya, kuhamasisha na kujenga uwezo wa jamii katika kujiletea maendeleo yao wenyewe.

Mafanikio ya TASAF ni halisi na yamegusa na kuleta matokeo kwa sehemu kubwa ya jamii katika nchi yetu, hususan, kwa maskini waliopo vijijini. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana TASAF inafahamika mahali popote katika nchi yetu.

Ni mategemeo yetu kwamba hali ya umiliki, ushiriki na uwazi ambayo imejengwa miongoni mwa jamii itawezesha kuwepo uendelevu katika rasilimali mbalimbali ambazo zimetokana na miradi inayotekelezwa kwa kuwezeshwa na TASAF. Aidha, natoa wito kwa wananchi kuutumia Mpango huu vizuri ili kuweza kufikia Azma ya Serikali ya Maisha Bora kwa Kila Mtanzania.

Ndugu wananchi
Wakati ninapohitimisha ningependa kutoa shukrani za pekee kwa Benki ya Dunia kwa mchango wa kitaalamu wa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 4.5, pamoja na Serikali ya Japan ambayo ilitoa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 1.9 ambazo zimewezesha kufanikisha maandalizi ya Mpango huu wa Kijamii wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini.

Aidha, Benki ya Dunia imekuwa ikitoa fursa mbalimbali kwa Menejimenti ya TASAF kujifunza kuhusu uanzishaji na utekelezaji wa programu kama hii kwenye nchi nyingine duniani.

Nichukue fursa hii pia kuishukuru Benki ya Dunia kwa ajili ya kupanua Mpango huu. Ni matarajio yetu kuwa Benki ya Dunia na wadau wengine wa maendeleo wataendelea kutuunga mkono kwa kutoa msaada wa kitaalamu na fedha pale utakapohitajika, vilevile kupanua Mpango huu, ikiwezekana utekelezwe katika Halmashauri zote nchini.

Ndugu wananchi
Baaada ya maelezo haya sasa natamka rasmi kuwa, Mpango wa Kijamii wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini umezinduliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Mhe. Sophia Simba (Mb) Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) kwenye uzinduzi wa Mpango wa Kijamii wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini, kiwanja cha Maili Moja Kibaha, Mkoa wa Pwani, 29 Septemba 2009